# UCHAGUZI

Jarida la Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Toleo Na. 22 Agosti, 2024

HALIUZWI



## Yaliyomo

- Waziri Mkuu azindua Uboreshaji-Kigoma
- Kadi zenye jina la Zamani ni halali
- Makabila, Linex, Msechu watikisa Uzinduzi-Kigoma




# WAZIRI MKUU AZINDUA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA

**Na Mwandishi Wetu**

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (MB) amezindua Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura katika hafla iliyofanyika katika uwanja wa Kawawa uliopo Manispaa ya Kigoma Ujiji mkoani Kigoma.

Mhe. Majaliwa baada ya kuzindua zoezi hilo amepata fursa ya kushuhudia kuandikishwa kwa mpiga kura na kumkabidhi kadi yake.

Akihutubia wananchi waliohudhuria hafla hiyo Mhe. Majaliwa amewataka raia wote wa Tazania wenye sifa wajitokeze kujiandikisha kuwa wapiga kura na kuhakikisha kuwa wasio raia wa Tanzania hawaandikishwi kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

“Nitoe rai kwa kila mpiga kura aliyeandikishwa mwenye uhitaji wa kuboresha taarifa iwe kwa kurekebisha taarifa au kuhama kutoka eneo moja la uchaguzi kwenda lingine asisite kufika katika kituo cha kuandikisha kwani Tume imeshajipanga ili kuhakikisha wananchi wote wanafikiwa”.

Aidha, Mheshimiwa Majaliwa amesema kuwa zoezi hilo lina lengo la kuhakikisha wananchi wote wenye sifa wanapata na kutumia haki yao ya kikatiba kama ilivyobainishwa kwenye Ibara ya 5 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Kadhalika Mheshimiwa Majaliwa amelitaka Jeshi la Magereza kuweka miundombinu wezeshi ili kuiwezesha Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi kutekeleza wajibu wake wa kuandikisha wafungwa wenye vifungo chini ya miezi sita na mahabusu kwa ufanisi.

“Hii fursa ambayo Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilipitisha sheria ya kuwawezesha magereza kupiga kura ya kuchagua viongozi wanaowataka, hii mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu kutoa fursa kwa wafungwa na mahabusu kupiga kura wakiwa magerezani”

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu amewahakikishia watanzania kuwa Rais Dkt Samia Suluhu Hassan amedhamiria kuhakikisha kuwa chaguzi zote zitakuwa huru na Haki.

Mhe. Majaliwa amesisitiza kuwa zoezi hilo ni kwa ajili ya maandalizi ya uchaguzi na kwamba wasio raia wa Tanzanai hawahusiki.

“..anayetakiwa kaundikishwa hapa ni raia wa Tanzania tu. Hapa ni lazima tuwe wazalendo. Tusiruhusu mtu yeyote kutoka nje kujandikisha kuwa mpiga kura,” amesema.

Mhe. Majaliwa pia amevitaka vyama vya siasa kutumia ruhusa ya kisheria ya kuwekamawakala kila kituo, kuhakikisha wanachagua mawakala ambao wanatoka kwenye maeneo vilipo vituo vya kuandikisha wapiga kura ili wawaze kuwatambua watu wanaojiandikisha na uraia wao.

“Mawakala wa vyama vya siasa mna wajibu wa kuwatambua wanaojiandikisha, naomba nisisitize hapa, lazima muwe wazalendo namba moja, uzalendo wenu utasaidia kuwatambua watu ambao sio raia.”

Kwa Upande wake, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) Ummy Nderiandanga amesema kuwa uzinduzi wa uandikishaji na uboreshaji, mchakato huo umeshirikisha wadau mbalimbali wa uchaguzi ikiwa ni utekelezaji wa falsafa ya 4R za Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

“Tume imekutana na wadau wa makundi mbalimbali kama vile Vyama vya Siasa, Asasi za Kiraia,Viongozi wa Dini, Makundi Maalum kama vile Vijana, Wanawake na watu wenye Ulemavu .Lengo ni kuhakikisha kuwa mchakato huu unakuwa shirikishi kwa watanzania wote bila kujali itikadi za vyama vya siasa au dini”

Naye, Mwenyekiti wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Jaji Jacobs Mwambegele amesema kuwa Jumla ya vituo 40,126 vitatumika katika zoezi la uboreshaji wa Daftari ambapo kati ya hivyo, vituo 39,709 vipo Tanzania Bara na vituo 417 vipo Tanzania Zanzibar.

“Idadi hii ya vituo ni ongezeko la vituo 2,312 zaidi ikilinganishwa na vituo 37,814 vilivyotumika kuandikisha Wapiga Kura kwa mwaka 2019/2020”.

Ifahamu Tume

# Sifa za kujiandikisha kuwa mpiga kura

**Ibara ya 5(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 ikisomwa pamoja na kifungu cha 9 cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na.1 ya Mwaka 2024 zimeainisha sifa za mtu kuandikishwa kuwa mpiga kura ambazo ni: -**

(i) raia wa Tanzania;

(ii) ametimiza umri wa miaka 18; na

(iii) awe hajapoteza sifa kwa mujibu wa sheria ya uchaguzi au sheria nyingine yoyote iliyotungwa na Bunge.

**Kukosa Sifa za Kuandikishwa Kuwa Mpiga Kura Kwa mujibu wa kifungu cha 10(1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na.1 ya Mwaka 2024, mtu atakosa sifa za kuandikishwa kuwa mpiga kura kwa sababu zifuatazo: -**

(i) si raia wa Tanzania;

(ii)yuko chini ya kiapo cha utii kwa nchi nyingine tofauti na Tanzania;

(iii) amethibitika kuwa hana akili timamu;

(iv) ametiwa hatiani kwa kosa ambalo adhabu yake ni kifo au anatumikia kifungo kwa kosa ambalo adhabu yake inazidi miezi sita iliyotolewa na Mahakama au kama ilivyobadilishwa na mamlaka yenye dhamana;

(v)amezuiliwa kujiandikisha kuwa mpiga kura na sheria za uchaguzi au sheria nyingine kwa makosa yanayohusiana na uchaguzi; na

(vi) hatakuwa ametimiza umri wa kupiga kura, ifikapo tarehe ya Uchaguzi Mkuu.

# HONGERA WANANCHI WA TABORA, KATAVI, NA KIGOMA KWA KUBORESHA TAARIFA ZENU

## Tahariri

Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura katika mikoa ya Kigoma, Tabora na Katavi umefanyika kuanzia tarehe 20 hadi 26 Julai, 2024 ambapo wananchi katika mikoa hiyo walipata fursa ya kujiandikisha kuwa wapiga kura wapya, ama kurekebisha, kuhamisha au kurekebisha na kuhamisha taarifa zao kwa wapiga kura waliokuwa na hitaji hilo.

Kujitokeza kwa wingi kushiriki katika uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ni ishara ya uzalendo walio nao wananchi katika kushiriki katika masuala mbalimbali ya kitaifa likiwemo suala hili la uboreshaji wa Daftari.

Hatua hii inadhihirisha utayari walio nao wananchi katika mikoa hii wa kushiriki katika Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani utakaofanyika mwaka 2025.

Tunapoisifu na kupongeza hatua muhimu iliyochukuliwa na wananchi wa mikoa ya Tabora, Katavi, na Kigoma, ni muhimu kuonyesha shukrani zetu kwa jitihada zenu za kujitokeza kwa wingi kujiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Kwa ushiriki wenu mkubwa, mmeonesha mfano wa kuigwa katika kukuza demokrasia nchini.

Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ni hatua muhimu kuelekea uchaguzi mkuu ujao na ni msingi wa kuhakikisha kwamba kila mtu mwenye sifa ya kujiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura anapata haki ya kupiga kura.

Ni muhimu kuelewa kwamba kila hatua ya ushiriki katika mchakato huu ina mchango mkubwa katika mustakabali wa nchi yetu. Kwa hivyo, jitihada zenu za kujiandikisha na kuboresha taarifa zenu katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura zinapaswa kupongezwa na jamii nzima ya Watanzania.

Kupitia uboreshaji wa Daftari katika mikoa hii tumeona jinsi wananchi wanavyoweza kutoa mchango mkubwa katika kuimarisha demokrasia.

Kwa kujitokeza kwa wingi kujiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura mmekuwa mfano kwa wananchi wa mikoa mingine ambayo itashiriki uboreshaji wa Daftari katika siku za usoni kulingana na ratiba ya Tume.

Hongereni sana kwa jitihada zenu wananchi wa Kigoma, Tabora na Katavi, na ni matumaini yetu kuwa kama vile mlivyojitokeza kujiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura pia mtajitokeza katika mchakato wa uchaguzi mkuu ujao wa Rais, Wabunge, na Madiwani utakaofanyika mwaka 2025.

Tunapongeza jitihada zenu na tunatarajia kwamba wananchi wa mikoa hii pia wanajitokeza pia katika kuwania nafasi mbalimbali za uongozi katika nchi yetu.

KUJIANDIKISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA!




**Endelea kufuatilia Kurasa za Mitandao ya Kijamii ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi pamoja na Tovuti ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, ili kupata habari zinazohusu Tume hususani katika kipindi cha Uboreshaji wa Daftari la kudumu la Wapiga Kura.**

# WANANCHI MIKOA YA KIGOMA, TABORA, NA KATAVI WAJITOKEZA KUBORESHA TAARIFA ZAO



**Na Mwandishi Wetu**

Wananchi katika Mikoa ya Kigoma, Tabora, na Katavi wamejitokeza kujiandikisha na kuboresha taarifa zao katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura mara baada ya uzinduzi kufanyika mkoani Kigoma mnamo tarehe 20 Julai, 2024.

Kwa mujibu wa ratiba, zoezi hili ambalo lilianza kwa kuhusisha mzunguko wa kwanza katika mikoa hiyo linatarajiwa kufanyika kwa mizunguko 13, ambapo kila mzunguko utadumu kwa siku saba.

Vituo vya kuandikisha wapiga kura vitafunguliwa kila siku saa mbili asubuhi (2:00) na kufungwa saa kumi na mbili jioni (12:00). Wananchi wanahimizwa kujitokeza kwa wingi ili kuandikisha taarifa zao kuandikishwa na kuboreshwa kwa usahihi.

Mara baada ya kukamilika katika mikoa hiyo uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura umepangwa kufanyika katika mikoa ya Kagera na Geita kuanzia tarehe 05 hadi 11 Agosti, 2024 na kisha katika mikoa ya Mwanza na Shinyanga kuanzia tarehe 21 hadi 27 Agosti, 2024.

Kwa upande wa Zanzibar, uboreshaji wa Daftari utafanyika kuanzia tarehe 07 hadi 13 Oktoba, 2024. Zoezi hili litamhusu kila mtu aliyepo Zanzibar ambaye hana sifa za kuandikishwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) lakini anayo sifa ya kumchagua Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kulingana na kifungu cha 13 (1) na (2) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge, na Madiwani Na. 1 ya mwaka 2024.

Uboreshaji wa Daftari hutanguliwa na kufanyika kwa mikutano ya wadau ambapo hadi kufikia sasa mikutano hiyo imekwishafanyika katika mikoa ya Kigoma, Tabora, na Katavi ambapo wadau wa uchaguzi katika mikoa hiyo walipata fursa ya kushiriki katika mikutano ni sehemu ya maandalizi ya uboreshaji wa Daftari katika mikoa hiyo.

Akifungua Mkutano wa wadau wa uchaguzi mkoani Kigoma mnamo Juni 19, 2024, Mwenyekiti wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Jaji wa Mahakama ya Rufaa Mhe, Jacobs Mwambegele aliwahimiza wadau hao kutumia majukwaa mbalimbali waliyo nayo kuwahimiza wafuasi wao kushiriki katika uboreshaji wa Daftari.

Mikutano kama hiyo pia ilifanyika katika mikoa ya Tabora na Katavi na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali wa uchaguzi wakiwemo viongozi wa vyama vya siasa, asasi za kiraia, viongozi wa Dini, wawakilishi wa makundi mbalimbali ya kijamii kama vile wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Makundi mengine ni pamoja na wahariri wa vyombo vya habari, waandishi wa habari, Maafisa Habari wa Mikoa, na halmashauri, na wazee wa kimila waliopo katika mikoa hiyo.

Kufanyika kwa mikutano hiyo ya wadau mikoani ni mwendelezo wa mikutano ya kitaifa ambayo ilifanyika jijini Dar es salaam kuanzia juni 7 hadi juni 15, 2024.

# KADI ZA MPIGA KURA ZENYE JINA LA ZAMANI LA TUME NI HALALI

**Na Mwandishi Wetu**

Kadi za mpiga kura zilizotolewa mwaka 2015 na 2020 ni halali na zitaendelea kutumika kwenye chaguzi kuu zijazo bila kujali mabadiliko ya jina la Tume ya Uchaguzi kutoka Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuwa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi.

Akizungumza wakati wa ziara aliyoifanya ya kukagua vituo vya kuandikishia wapiga kura tarehe 22 Julai, 2024 katika Halmashuari ya Wilaya ya Kasulu, Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, Bw. Kailima Ramadhan amesema wapiga kura wenye kadi hizo hawahusiki na zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

“Naomba nitoe wito kwa wale ambao kadi zao ni zile zenye jina la Tume ya Taifa ya Uchaguzi na wanadhania kuwa kubadilika kwa jina la Tume kunasababisha kubadili kadi watambue kuwa kadi zao ni halali kwa mujibu wa kifungu cha 168 cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024,” amesema.

Mkurugenzi huyo wa uchaguzi ambaye kwenye ziara yake aliambatana na Afisa Mwandikishaji wa Jimbo la Kasulu Vijini, Bw. Emmanuel Ladislaus na maafisa wengine waandamizi, alieleza kwamba wenye kadi hizo ambazo zimeharibika, zimepotea au wamehama kutoka eneo moja la uchaguzi kwenda eneo lingine wanahusika kwenye zoezi hilo.

“Nimebaini kuwa wapo wapiga kura wenye kadi za zamani zilizotolewa kabla ya mwaka 2015 (zile za karatasi) hao waje vituoni ili waandikishwe upya kwa kuwa mfumo uliotumika wakati huo ni tofauti na mfumo wa sasa,” amesema.

Uboreshaji wa Daftari katika mikoa hiyo umefanyika tarehe 20 hadi 26 Julai 2024 ambapo vituo hufunguliwa kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi 12:00 jioni kila siku katika siku saba zilizotengwa kulingana na ratiba ya Tume.



“Kujiandikisha kuwa Mpiga Kura ni msingi wa uchaguzi bora”

# TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI YAZINDUA KITUO CHA HUDUMA KWA MPIGA KURA




**Na Mwandishi Wetu, Kigoma**

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), imezindua rasmi kituo cha huduma kwa mpiga kura lengo ni kuwawezesha wapiga kura na wale wanaotarajiwa kuandikishwa au kuboresha taarifa zao kupata ufafanuzi, majibu, na maelezo ya maswali au hoja zinazohusu zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

Mwenyekiti wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), Jaji wa Mahakama ya Rufaa, Mheshimiwa Jacobs Mwambegele amesema kituo hiki kimeanzishwa ili kuboresha huduma kwa wapiga na kwamba huduma hii, ambayo ni bure, ilianza kutolewa tarehe 18 Julai, 2024, ambapo mtu yeyote anakaribishwa kupiga namba 0800112100 na kupatiwa huduma hiyo ndani ya dakika 20.

Jaji Mwambegele amesema Tume imefanya maboresho makubwa katika mifumo ya uandikishaji.

"Wananchi waliopo kwenye Daftari sasa wanaweza kuanzisha mchakato wa kuboresha taarifa au kuhamisha taarifa zao wakiwa nje ya kituo cha kuandikisha wapiga kura kwa njia ya kielektroniki kwa kutumia simu ya mkononi au kompyuta," ameeleza Jaji Mwambegele na kuongeza kuwa baada ya kuanzisha mchakato huo, wananchi wanatakiwa kufika kituo cha kuandikisha wapiga kura kukamilisha mchakato huo kwa kuweka saini, kupigwa picha, na kupokea kadi yao ya mpiga kura.

Tume pia imezingatia maoni ya wadau mbalimbali, ambao waliomba mfumo huu uwezeshe pia wenye simu za kawaida (maarufu kama kitochi) kuanzisha mchakato wa kuboresha au kuhamisha taarifa zao. Kuanzia tarehe 20 Julai, 2024, huduma hii inapatikana kwa kupiga SSD Code *152*00# na kubonyeza namba 9, kisha kufuata maelekezo kwenye simu husika.

Uzinduzi wa kituo hiki cha huduma kwa mpiga kura ni sehemu ya juhudi za Tume katika kuhakikisha kuwa zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura linafanyika kwa ufanisi na uwazi. Kwa mujibu wa Mwenyekiti Mwambegele, jumla ya vituo 40,126 vitatumika katika zoezi hili la uboreshaji. Kati ya hivyo, vituo 39,709 vipo Tanzania Bara na vituo 417 vipo Tanzania Zanzibar. Idadi hii ni ongezeko la vituo 2,312 zaidi ikilinganishwa na vituo 37,814 vilivyotumika kuandikisha wapiga kura katika mwaka wa 2019/2020.

Mwenyekiti Mwambegele alibainisha pia kuwa Tume imefanya maandalizi ya vifaa muhimu kwa ajili ya uboreshaji huu, ikiwa ni pamoja na ununuzi wa BVR Kits 6,000 zinazotumia programu endeshi ya android na zenye uzito wa kilo 18, pamoja na vifaa vingine kama kadi mpya, wino, na makasha ya kubebea vifaa na fomu mbalimbali za uboreshaji.

Katika jitihada za kuimarisha ushirikiano na wadau, Tume imeshakutana na wadau muhimu wa uchaguzi, wakiwemo vyama vya siasa, wawakilishi wa wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu, kwa lengo la kubadilishana mawazo na kuwapa taarifa za mchakato wa uboreshaji. Mikutano hii imefanyika katika mikoa mbalimbali na itaendelea kufanyika katika mikoa yote ya Tanzania.

Aidha, Tume imeendelea kutoa elimu kwa wapiga kura kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii. Vibali vimetolewa kwa taasisi na asasi 157 zitakazotoa elimu ya mpiga kura na vibali vingine kwa taasisi na asasi 41 za ndani na nje ya nchi kuwa waangalizi wa uandikishaji.

Mwenyekiti Mwambegele alisisitiza kuwa Tume itaendelea na wajibu wake wa kuhakikisha kuwa zoezi hili linaendeshwa kwa uwazi na ufanisi, huku akihimiza ushirikiano wa karibu na wadau wote wa uchaguzi.

# VIBALI VYA ELIMU NA WAANGALIZI KIELELEZO CHA UWAZI KWENYE UBORESHAJI WA DAFTARI

**Na Mwandishi Wetu**

Kila jambo linalowahusu wananchi na ambalo lina maslahi kwa umma linapaswa kufanywa kwa uwazi na kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali. Ni kutokana na ukweli huo Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi wakati huu wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura imewashirikisha wadau kwa kiasi kikubwa katika hatua mbalimbali.

Mathalani, katika hatua za mwanzo kabisa kuelekea kwenye zoezi hilo la uboreshaji wa Daftari ambalo limezinduliwa tarehe 20 Julai, 2024 mkoani Kigoma ambapo mgeni rasmi alikuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (MB), Tume imeshirikisha wadau kadhaa.

Wadau hao ni pamoja na Vyama vya Siasa, Viongozi wa Dini, Taasisi na Asasi za Kirai, Wahariri wa Vyombo vya Habari, Waandishi wa Habari, Makundi Mbambalimbali ya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu na Wazee wa Kimila.

Katika kuendeleza na kuimarisha uwazi kwenye zoezi hilo wakati akizungumza kwenye uzinduzi wa zoezi hilo mkoani Kigoma, Mwenyekiti wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, Mhe. Jaji (Rufaa) Jacobs Mwambegele alisema kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 10(1)(h) cha Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Na. 2 ya mwaka 2024, Tume imetoa vibali kwa taasisi na asasi 157 zitakazotoa elimu ya mpiga kura katika kipindi chote cha uboreshaji.

"Aidha, kwa kuzingatia dhana ya uwazi katika zoezi hili pamoja na masharti ya kanuni ya 46(1) na (4) ya Kanuni za Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura za Mwaka 2024, Tume imetoa vibali kwa taasisi na asasi 33 za ndani kuwa waangalizi wa uandikishaji kwa ajili ya kutazama uendeshaji wa zoezi la uboreshaji," alisema Jaji Mwambegele.

Alisema taasisi na asasi zote zilizopewa kibali cha kutoa elimu ya mpiga kura na uangalizi wakati wa zoezi la uboreshaji, zimepewa nyaraka mbalimbali ikiwemo Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Sheria na miongozo inayosimamia jukumu la utoaji wa elimu ya mpiga kura na utazamaji katika zoezi hilo.

"Tume itaendelea na wajibu wake kuhakikisha taasisi na asasi hizo zinatekeleza wajibu wao kwa mujibu wa sheria na kanuni," amesema Jaji Mwambegele.

Kutokana na maelezo hayo ya Jaji Mwambegele, Waziri Mkuu akasisitiza juu ya umuhimu wa taasisi na asasi hizo zilizopewa vibali kuhakikisha kuwa zinafanya kazi kwa kuzingatia Katiba, sheria mbalimbali za nchi, kanuni na maelekezo ya Tume.

"...taasisi na asasi zote zilizopewa vibali vya kutoa elimu ya mpiga kura na zile zilizokubaliwa kuwa waangalizi wakati wa zoezi hili la uboreshaji, zihakikishe zinatekeleza kazi zao kwa kuzingatia masharti ya vibali na miongozo iliyotolewa na itakayotolewa na Tume,"alisema Mhe. Majaliwa.

Alizitaka taasisi na asasi hizo za kiraia zitambue uwepo wa sheria nyingine za nchi kwa kuwa sheria hizo zinaendelea kufanya kazi na kibali kisiwe kisingizio cha ukiukwaji wa sheria zingine kwa namna yoyote ile.



# UMUHIMU WA UZALENDO KWENYE UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA

**Na Mwandishi Wetu**

"Kila Mtanzania ashiriki katika usimamizi wa suala hili kwani wanaotakiwa kuandikishwa ni raia wa Tanzania tu wenye sifa zilizobainishwa kwa mujibu wa sheria. Wananchi ni watambuzi wa kwanza, niwasihi sana tuwe wazalendo, huu ni wajibu wa raia wa Tanzania kuhakikisha wanaoandikishwa ni Watanzania tu," ni kauli ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa aliyoitoa tarehe 20 Julai, 2024 pale Uwanja wa Kawawa mkoani Kigoma wakati akizindua uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

Ni wazi kuwa Waziri Mkuu pamoja na mambo mengine aliyoyazungumzia siku ile ya uzinduzi, "uzalendo" kwenye mchakato wa kuboresha Daftari lilikuwa jambo kuu lililotawala hotuba yake, alitumia muda mwingi sana kusisitiza uzalendo kwenye zoezi hilo kwa kuwa nchi yetu ya Tanzania ni kubwa, imepakana na nchi nyingi za Afrika na pia uwepo wa amani na utulivu unaifanya kuwa kimbilio la wengi, hivyo, suala la uzalendo kwenye mazoezi kama haya ni muhimu sana vinginevyo wasiokuwa raia wa Tanzania wanaweza kujipenyeza.

Ikumbukwe kuwa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi kwa mujibu wa ibara ya 74(6) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ikisomwa pamoja na kifungu cha 10(1)(a) na (b) cha Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Na. 2 ya mwaka 2024, imepewa majukumu kadhaa ikiwemo kusimamia na kuratibu uandikishaji wa wapiga kura kwa ajili ya uchaguzi wa Rais na Wabunge katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Madiwani kwa Tanzania Bara.

Vilevile, kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 16(5) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya mwaka 2024, Tume ina wajibu wa kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura mara mbili kati ya kipindi kinachoanza baada ya uchaguzi mkuu mmoja na kabla ya siku ya uteuzi wa uchaguzi mkuu unaofuata.

Na kwa kuwa, mara ya mwisho Tume kuboresha Daftari ilikuwa mwaka 2019/2020 ni muda sasa wa kuboresha Daftari na hii ni awamu ya kwanza, ambayo kwa mujibu wa taarifa mbalimbali zilizotolewa na Tume uboreshaji huo wa awamu ya kwanza utakamilika mwezi Machi 2025.

Ikumbukwe kuwa baada ya kukamilika kwa awamu hiyo ya kwanza, Tume itaweka wazi Daftari la awali kwa ajili ya watu wanaotambulika kisheria wakiwemo wapiga kura kulikagua.

Kutokana na hilo, Waziri Mkuu anasisitiza "ni wajibu wetu sisi sote Watanzania kutumia nafasi hii kulikagua Daftari la Awali litakapowekwa wazi na kutoa taarifa iwapo kuna watu, ambao tunadhani hawana sifa kama vile wasio raia wa Tanzania na tayari kwa bahati mbaya wameshaandikishwa, ili waweze kuondolewa kwenye Daftari kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa".

Mhe. Majaliwa alilitaka Jeshi la Uhamiaji liwajibike kutoa elimu kwa wananchi kuhusu kuwatambua na kutoa taarifa za uwepo wa mtu au watu ambao siyo raia wa Tanzania, walioandikishwa tayari au wanaopanga kwenda kuandikishwa ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa mapema dhidi yao.

Kwa upande wa vyama vya siasa, Waziri Mkuu alivitaka vyama kutumia fursa ya kisheria kuweka mawakala wa uandikishaji kwenye kila kituo cha uandikishaji chini ya kifungu cha 17(1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya mwaka 2024.

"Ninatoa rai kwa viongozi wa vyama vya siasa kuhakikisha mawakala wao wanatoka kwenye mtaa, kijiji na shehia husika ili waweze kutimiza wajibu wao wa kisheria wa kuwatambua watu wenye sifa za kuandikishwa kuwa wapiga kura. Iwapo hili litafanyika ipasavyo, uwezekano wa kuandikisha wapiga kura ambao siyo raia wa Tanzania halitakuwepo," alisema Mhe. Majaliwa.

Wajibu wa uzalendo kwenye zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura upo pia kwa mawakala watakaoteuliwa kwa kuwa wao ndio wanawafahamu watu wanaoishi kwenye maeneo yao. Hivyo, Waziri Mkuu alisisitiza juu ya umuhimu wa mawakala hao kuwa wazalendo wakati wakitekeleza majukumu yao.

"Mawakala watakaoteuliwa na vyama vya siasa nao wanaowajibu wa kutambua wenye sifa za kuandikishwa wanaofika kwenye kituo kwa ajili ya kuandikishwa kuwa wapiga kura. Niwasisitize mawakala wote wawe wazalendo, lakini pia wawe na imani na chombo kilichopewa jukumu la kusimamia zoezi hilo hapa nchini," alisema.

Uzalendo ukasisitizwa pia kwa watendaji mbalimbali walioteuliwa na Tume kuendesha zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura haswa katika kujituma na kuwahudumia wananchi kwa ufanisi na weledi.

"Ninawasihi sana watendaji walioteuliwa na Tume kuanzia ngazi ya mkoa, jimbo, kata na kituo cha kuandikisha wapiga kura kuwa waadilifu na watangulize uzalendo kwa kutotoa fursa kwa watu ambao hawana sifa za kushiriki katika uboreshaji. Kila mmoja ajitume, afanye kazi kwa weledi na kutumia lugha nzuri wakati wote wa utekelezaji wa majukumu aliyopangiwa," alisema Mhe. Majaliwa.

Katika kutekeleza hayo, Waziri Mkuu aliwataka watendaji hao kuhakikisha wanazingatia sheria, kanuni na miongozo itakayotolewa na Tume, ili kufanikisha zoezi hilo muhimu kwa mustakbali wa Taifa.

# DULLA MAKABILA, LINEX WATIKISA TAMASHA LA UBORESHAJI DAFTARI



**Na Mwandishi Wetu,**

Wasanii maarufu wa muziki wa Bongo Fleva na Singeli, Sande Mangu, maarufu kama Linex, na Abdallah Ahmed, maarufu kama Dulla Makabila, waliwapa burudani ya nguvu wakazi wa Kigoma mnamo Julai 18, 2024.

Tukio hili lilikuwa ni sehemu ya Tamasha la Uzinduzi wa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura lililoandaliwa na Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC).

Uzinduzi rasmi wa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura umefanyika Julai 20, 2024, katika Uwanja wa Kawawa, Ujiji Kigoma, ambapo mgeni rasmi alikuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa.

Linex, ambaye ni mzaliwa wa Kigoma, alikuwa wa kwanza kupanda jukwaani na kuwashirikisha mashabiki wake kwa nyimbo maarufu, ikiwemo wimbo maalum wa kuhamasisha wananchi kujitokeza kuboresha taarifa zao na kujiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

Linex pia aliimba wimbo wake maarufu "Mahakama ya Mapenzi" pamoja na kibao maarufu "Leka Dutigite," alichoimba na kundi la Kigoma All Stars.

Baada ya Linex, Dulla Makabila alipanda jukwaani na kutoa burudani kwa nyimbo zake maarufu kama "Pita Huku," "Furahi," na "Hujaulamba," pamoja na nyimbo za Simba na Yanga ambazo ziliwasha moto jukwaani. Msanii Dulla Makabila alipata fursa ya kutumbuiza katika halfa ya uzinduzi wa uboreshaji wa Daftari ambao umefanyika tarehe 20 Julai, 2024 mjini Kigoma.

Wananchi waliohudhuria katika viwanja vya Kawawa, Kigoma Ujiji, walifurahia burudani hiyo, na pia vikundi mbalimbali vya burudani kama Warumba Shauri, Smart Boys, Vijana Rumba, Chama Dansa, Mwandiga One, na Waobama vilitoa shoo za kuvutia

Kundi la Waobama liliibuka washindi kati ya vikundi vya dansi vilivyoshindana, na walikabidhiwa zawadi na Mkurugenzi wa Habari na Elimu ya Mpiga Kura, Bi. Giviness Aswile.

# KITUO CHA HUDUMA KWA MPIGA KURA

**Kuanzia Saa 12:00 Asubuhi**
**Hadi Saa 02: usiku**

**0800 112 100**




**"Kujiandikisha Kuwa Mpiga Kura ni Msingi wa Uchaguzi Bora"**

www.inec.go.tz
tumeyauchaguzi_tanzania
tumeyauchaguzi_tanzania
Tume ya Uchaguzi-TZ
Tume Huruya TaifayaUchaguzi
Uchaguzi TV
Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi





**Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi**
**Makao Makuu Dodoma,**
**5 Barabara ya Uchaguzi,**
**41107 Njedengwa,**
**Uchaguzi House,**
**Anuani: S.L.P 358, Dodoma**
**Namba ya simu: +255 26 2962345-8**
**Nukushi: +255 26 2962348**
**Barua pepe: Uchaguzi@inec.go.tz**

www.inec.go.tz
tumeyauchaguzi_tanzania
Tume ya Uchaguzi-TZ
Tume ya Uchaguzi-tz
Uchaguzi TV